**Nambari ya Mtahiniwa ___________________**

**SMZ**

**BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR**

**MTIHANI WA KUINGILIA KIDATO CHA TATU**

**021 KISWAHILI**

**MUDA: SAA 2:30 JUMATATU 03/12/2018 mchana**

---

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**

1. **Mtihani huu una sehemu NNE (4) A, B, C, na D.**
2. **Jibu maswali YOTE kutoka sehemu A, maswali MAWILI (2) kutoka sehemu B, maswali MAWILI (2) kutoka sehemu C na swali MOJA (1) kutoka sehemu D.**
3. **Andika nambari yako ya mtihani katika kila ukurasa.**
4. **Majibu yote yaandikwe kwenye sehemu zilizoachwa wazi.**
5. **Simu za mkononi haziruhusiwi ndani ya chumba cha mtihani.**

| KWA MATUMIZI YA WASAHIHISHAJI | | |
|---|---|---|
| **NAMBARI YA SWALI** | **ALAMA** | **SAINI** |
| 1. | | |
| 2. | | |
| 3. | | |
| 4. | | |
| 5. | | |
| 6. | | |
| 7. | | |
| 8. | | |
| 9. | | |
| 10. | | |
| JUMLA | | |

**Mtihani huu una kurasa 15 zenye maandishi**

**Nambari ya Mtahiniwa ________________**

## SEHEMU A: (Alama 20)

## UFAHAMU

**Jibu maswali YOTE katika sehemu hii**

1. **Soma kwa makini habari ifuatayo kisha jibu maswali yanayofuata.**

Mama Baraka aliwaita watoto wake wa kiume Baraka na Mbaruku, akawaambia "Wanangu nimewaita hapa nilipolala kwa lengo la kuwajuza mambo muhimu". Baraka na Mbaruku walikaa vizuri ili wamuazime masikio yao. Mama yao aliendelea kwa kusema. "Jambo la kwanza napenda kuwaambia kuwa leo ni siku ya mwisho kuwa nanyi katika dunia hii". Watoto kusikia hivyo walitaharuki na kububujikwa na machozi. Mama alivuta pumzi huku akiwaangalia watoto wake kwa jicho la huzuni.

Mama aliendelea kuwaeleza wanawe jambo jengine kuwa, "Muwapo duniani mjihadhari na wale wanaovaa ngozi ya kondoo juu ya ngozi ya chui, watu hao ni maadui kwenu, msiwaamini hata kidogo. Wakale walisema kuwa subira huvuta kheri na haraka haraka haina baraka lakini tunatakiwa tufikirie hasara ya yote hayo. Wanangu mchukuwe tahadhari mapema msije kujiingiza kwenye dimbwi la dhulma".

Baada ya hapo mama Baraka aliwaangalia watoto wake kwa huzuni kisha akasema "Jambo la mwisho wanangu, ninawaacha katika maisha magumu kwani sina nyumba nzuri ya kuwaachia zaidi ya kibanda". Ghafla mama Baraka alivuta pumzi ndefu na kuzishusha hatimae aliaaga dunia. Baraka na Mbaruku walibaki katika wimbi zito la huzuni.

**MASWALI.**

a) Ni sababu ipi iliyomfanya mama Baraka kuwaita watoto wake?

________________________________________

________________________________________

b) Jambo gani lililowafanya Baraka na Mbaruku kububujikwa na machozi?

________________________________________

________________________________________

c) Andika methali mbili (2) alizozitaja mwandishi katika habari hii.

_______________________________________________

_______________________________________________

d) Toa kichwa cha habari kisichozidi maneno matatu (3) kuhusu habari uliyoisoma.

_______________________________________________

e) Eleza maana ya maneno au kifungu cha maneno yafuatayo kama yalivyotumika kwenye habari uliyoisoma.

i. Kuwajuza

_______________________________________________

_______________________________________________

ii. Walitaharuki

_______________________________________________

_______________________________________________

iii. Wanaovaa ngozi ya kondoo juu ya ngozi ya chui

_______________________________________________

_______________________________________________

iv. Kuaga dunia

_______________________________________________

_______________________________________________

2. Fupisha aya ya mwanzo ya habari uliyoisoma kwa maneno yasiyozidi ishirini (20).

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

Nambari ya Mtahiniwa ___________________

## SEHEMU B: (Alama 30)

## SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA

**Jibu maswali MAWILI (2) katika sehemu hii. Swali la tano (5) ni la lazima**

3. a) Zipange nomino zifuatazo katika aina zake.

Maji, jeshi, ujinga, mafuta, zimwi, bunge

| Nomino za jamii | Nomino za dhahania | Nomino za wingi |
|---|---|---|
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |

b) Bainisha vielezi katika sentensi zifuatazo:-

i. Nimekuonya mara tano lakini husikii.

_______________________________________________

ii. Siku hizi vitu vingi vimepanda bei.

_______________________________________________

c) Tunga sentensi ukitumia vihisishi vifuatavyo:

i. Mashallahi!

_______________________________________________

_______________________________________________

ii. Loo!

_______________________________________________

_______________________________________________

d) Eleza aina mbili (2) za vitenzi halisi huku ukitoa mfano mmoja mmoja kwa kila aina.

i. _______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

ii. _______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

e) Tofautisha kwa kutumia mifano kati ya vivumishi viulizi na vivumishi vioneshi.

______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

4. a) Badilisha vitenzi vifuatavyo katika kauli ya kutendwa.

i. Omba ______________________________________________________

ii. Sahau ______________________________________________________

b) Onesha mzizi katika maneno yafuatayo:

i. Tuliyoyaona

______________________________________________________________

ii. Wanaandikiana

______________________________________________________________

c) i. Nini maana ya sarufi?

______________________________________________________________
______________________________________________________________

ii. Eleza kwa ufupi tanzu nne (4) za sarufi.

______________________________________________________________
______________________________________________________________
______________________________________________________________
______________________________________________________________
______________________________________________________________
______________________________________________________________
______________________________________________________________

d) Kwa kutumia mifano eleza maana ya istilahi zifuatazo:

i. Mzizi funge

ii. Mofimu

e) Kwa kutumia mifano fafanua jinsi ya kuunda maneno yafuatayo kwa njia ya unyambuaji.

i. Vielezi kutokana na vivumishi

ii. Vitenzi kutokana na vielezi

5. a) Taja njia zilizotumika kuunda misimu ifuatayo:

   i. Malapa

   ______________________________________________________________

   ii. Fegi

   ______________________________________________________________

   b) Fafanua mambo mawili (2) yanayoathiri lafudhi na matamshi sahihi ya lugha ya Kiswahili.

   i. ______________________________________________________________

   ______________________________________________________________

   ______________________________________________________________

   ______________________________________________________________

   ii. ______________________________________________________________

   ______________________________________________________________

   ______________________________________________________________

   ______________________________________________________________

   c) Eleza aina mbili (2) za rejesta.

   i. ______________________________________________________________

   ______________________________________________________________

   ______________________________________________________________

   ii. ______________________________________________________________

   ______________________________________________________________

   ______________________________________________________________

   d) Orodhesha sifa tatu (3) za kamusi bora.

   i. ______________________________________________________________

   ii. ______________________________________________________________

   iii. ______________________________________________________________

e) Toa sababu tatu (3) zinazoonesha udhaifu wa lugha ya mazungumzo.

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

## SEHEMU C: (Alama 30)

## FASIHI

**Jibu maswali MAWILI (2) katika sehemu hii.**

6. Tunga beti mbili (2) za shairi la kimapokeo, kisha eleza vipengele viwili (2) vya fani ulivyovitumia katika beti hizo.

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

7. a) Eleza umuhimu wa uhakiki wa kazi za fasihi simulizi.

i.

ii.

b) Kwa kutumia mifano toa maana ya tamathali za semi zifuatazo:

i. Sitiari

ii. Tashihisi

c) Taja vipera viwili (2) vya hadithi.

i. ______________________________________________

ii. ______________________________________________

d) Eleza mambo mawili (2) yanayoonesha kufanana kwa Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi.

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

e) Kamilisha methali zifuatazo, kisha toa funzo tunalolipata kwa kila methali.

i. Akufaaye ........................................................................................

Funzo:

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

ii. Ukupigao ........................................................................................

Funzo:

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

8. a) Toa tofauti kati ya falsafa na maudhui.

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

b) Kwa kutumia mifano fafanua dhima zifuatazo za fasihi.

i. Kuhifadhi na kurithisha amali za jamii.

_________________________________________________________

_________________________________________________________

_________________________________________________________

_________________________________________________________

_________________________________________________________

_________________________________________________________

ii. Kukuza na kuendeleza lugha.

_________________________________________________________

_________________________________________________________

_________________________________________________________

_________________________________________________________

_________________________________________________________

_________________________________________________________

c) Taja mitindo miwili (2) ya mashairi ya fasihi simulizi.

i. _________________________________________________________

ii. _________________________________________________________

d) Eleza maana ya dhana za fasihi zifuatazo.

i. Sanaa

_________________________________________________________

_________________________________________________________

_________________________________________________________

_________________________________________________________

ii. Mandhari

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

e) Eleza faida mbili (2) za kuhifadhi kichwani kazi za fasihi simulizi.

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

**SEHEMU D: (Alama 20)**

**UANDISHI**

**Jibu swali MOJA (1) tu katika sehemu hii**

9. Andika Insha ya wasifu isiyopungua maneno 120 na isiyozidi maneno 130 kuhusu moja ya mada zifuatazo:

- Zao la karafuu Zanzibar
- Kilimo cha mbogamboga

Au

Eleza kwa kina mambo muhimu yasiyopungua matano (5) ambayo hupaswa kuzingatiwa katika uandishi wa Insha ya hoja.

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

10. Barua ya kuomba kazi ni moja kati ya aina za barua rasmi. Taja aina nyengine mbili (2) za barua rasmi, kisha andika mfano mmoja wa barua (rasmi) kati ya aina mbili za barua ulizozitaja. (Tumia nambari yako ya mtihani badala ya jina lako).

**Nambari ya Mtahiniwa** ____________________

.................................................